**HOTUBA YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGOLO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA, KWENYE UZINDUZI WA ZOEZI LA UGAWAJI WA VYANDARUA KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI.**

- ***Katibu Tawala Mkoa,***
- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,***
- ***Wakuu wa vyombo vya Usalama ngazi ya Mkoa,***
- ***Watendaji ngazi ya Sekretarieti ya Mkoa,***
- ***Wawakilishi wa Wizara ya Afya na TAMISEMI,***
- ***Viongozi wa Dini,***
- ***Wawakilishi wa Wazee wa Mkoa wa Rukwa,***
- ***Wakuu wa vyombo vya Usalama ngazi ya Wilaya,***
- ***Wakurugenzi wa Halmashauri,***
- ***Watendaji wa Halmashauri,***
- ***Wana Habari,***
- ***Mabibi na Mabwana,***

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....**

Awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo. Pia nichukue fursa ya kuwashukuru nyote mliofika hapa kwa ajili ya shughuli hii muhimu.

***Ndugu Washiriki,*** Serikali ya Mkoa wa Rukwa kwa kushirikiana na Serikali Kuu na Wadau mbalimbali wa maendeleo, katika kulinda afya za wananchi imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali za Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii. Moja ya maeneo ambayo yanatiliwa mkazo ni udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza hususan **Ugonjwa wa Malaria**.

***Ndugu Washiriki,*** Katika kukabiliana na changamoto ya ugonjwa wa Malaria, Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais –TAMISEMI na wadau wa Maendeleo imepanga kutekeleza Kampeni za Ugawaji wa Vyandarua kwa wanafunzi wa shule za Msingi ndani ya Mkoa wetu wa Rukwa.

***Ndugu washiriki,*** Kama mnakumbuka, hapo awali ugonjwa wa Malaria ulikuwa ni ugonjwa tishio ambao ulikuwa ukisababisha watu wengi kuugua na kusababisha vifo hasa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano na akina mama wajawazito katika Mkoa. Hali hiyo ya kuugua ugonjwa wa Malaria imekuwa ikipungua siku hadi siku kutokana na afua mbalimbali zinazofanywa na watendaji wetu kutoka ngazi ya Mkoa, Halmashauri na vituo vya kutolea huduma za Afya.

***Ndugu Washiriki,*** Natambua pia afua ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Mkoa katika kupambana na ugonjwa ambazo ni pamoja na kufanya uchunguzi kwa wagonjwa ili kubaini uwepo wa vimelea vya malaria na kutoa matibabu**, ugawaji vyandarua kwa akina mama wajawazito na watoto wachanga na kugawa vyandarua kwenye makundi maalum ikiwemo wazee.**

***Ndugu Washiriki,*** Serikali kwa kutambua juhudi mbalimbali tunazochukua kupambana na Malaria, imeamua kuongeza kasi ya upatikanaji wa vyandarua ngazi ya kaya kwa kugawa vyandarua kwa **wanafunzi 298,206** wa shule zote za Msingi za Umma na za Binafsi, za kutwa na za bweni. Zoezi hili ni endelevu kwani litafanyika kila baada ya mwaka na linachukua nafasi ya mazoezi ya ugawaji vyandarua moja kwa moja kwenye kaya ambapo zoezi kama hili lilifanyika mara ya mwisho mwaka jana mkoani kwetu**.**

***Ndugu Washiriki,*** Ninyi ni viongozi na kila mmoja anawakilisha kundi kubwa la watu anaowasimamia. Naomba kuchukua fursa hii kutoa rai yangu kwenu; mkatoe taarifa sahihi ili kuongeza uelewa kwa jamii na katika taasisi mnazotoka ili wananchi wavipokee na kuvitumia kila wakati vyandarua hivi ili kujikinga dhidi ya mbu waambukizao Malaria. Vyandarua hivi, vimethibitishwa kuwa ni salama kwa matumizi ya binadamu na

vinatengenezwa hapa hapa nchini na kiwanda cha A to Z kilichopo mjini Arusha.

***Ndugu Washiriki,*** Naomba tukawaeleze wananchi wapuuze habari zote za upotoshaji kuwa vyandarua hivi vina madhara ya kiafya kwani Serikali hujiridhisha juu ya usalama wa bidhaa zote kabla ya kuruhusu matumizi yake kwa wananchi. Pia tusivitumie vyandarua hivi kufugia kuku wala kuvulia samaki kwani havikukusudiwa kwa ajili ya matumizi hayo.

***Ndugu Washiriki,*** Pamoja na zoezi hili la ugawaji vyandarua ambalo tunalitarajia kuanza rasmi mwezi huu Oktoba na Novemba naomba tushiriki kuhamasisha jamii kuchukua tahadhari za kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Malaria kwa kuendelea kufanya yafuatayo:

- Kufukia madimbwi ya maji yaliyotuama au kunyunyiza dawa za kuua viluilui
- Kuondoa vitu vote vinavowezesha maji kutuama na kuwa mazalia ya mbu kama vile makopo na magurudumu chakavu ya magari.
- Kufyeka vichaka na nyasi zilizo karibu na makazi ya watu
- Kuhakikisha vyombo vyote vya kuhifadhia maji vinakuwa na mifuniko thabiti.
- Kufunika mashimo ya maji taka kwa mifuniko imara
- Kuvaa mavazi yanayofunika sehemu kubwa ya mwili wako

- Kuweka vizuizi vya mbu majumbani kama nyavu na kutumia vyandarua.
- Kama una uwezo nunua na upake dawa zinazoweza kuzuia mbu kukukaribia.

Nisisitize zaidi kufika haraka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya mara mpatapo dalili za homa ili muweze kuchunguzwa kama una malaria ili kupata tiba haraka.

***Mwisho,*** nirudie kuwashukuru Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Taifa wa kuthibiti Malaria na watendaji mbalimbali kutoka katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri kwa kazi kubwa ya kuratibu zoezi hili na mengine ya Kitaifa. Nawashukuru wote kila mmoja kwa nafasi yake ambaye anaendelea kuchangia katika afua ya Ugawaji wa vyandarua na mapambano dhidi ya Malaria.

**Mungu Ibariki Tanzania,**

**Mungu bariki Mkoa wetu wa Rukwa**

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.**

Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**